**LEARNING BY EAR 2012**

**“Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”**

**EPISODE 10: “Mwanzo mpya”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: KAPAKA NYUMBANI KWAKE NA FAMILIA**

- **Kapaka (MUME, 25)**
- **Cheupe (MKE, 25)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE TWO: TRIZA , MALEMBA NA CHUMBA KATIKA “ AUTISM CLUB”**

- **Malemba (MKE, 35)**
- **Triza (MKE, 30)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE THREE: IRENE AMTEMBELEA VALERIE HOSPITALI YA**

**WENDA WAZIMU**

- **Valerie (MKE, 19)**
- **Irene (MKE, 19)**
- **Mahiro (MUME, 50)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE FOUR: MAKAMO WA RAIS ASOMA BAJETI BUNGENI**

- **MAKAMU WA RAIS (MKE, 55)**
- **UMATI (KAMA WATU 5, UMRI NA JINSIA MCHANGANYIKO)**

**UTANGULIZI:**

Nakusalimu popote ulipo na karibu tena katika kipindi cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hiki ndicho kipindi cha kumi na cha hatima katika hadithi, **“Bado ningali mwanadamu”,** Hadithi hii inaangazia matatizo yanayowapata waathiriwa wa maradhi ya akili barani Afrika, kutokana na mafikira duni kuhusu wagonjwa hao . Kipindi tulichokihitimisha, Chumba, alijiunga na wenzake wenye maradhi kama yake, na alilakiwa kwa heshima na taadhima alipowasili pamoja na mamake kituoni hapo. Mwanafunzi wa uuguzi Valerie alipelekwa kwenye hospitali ya akili ili kutibiwa na kuangaliwa hali yake, ilhali Kapaka aliyekuwa kapoteza kazi yake, alirudi nyumbani na taarifa ya kupata tena ajira. Lakini haya yalijiri vipi, usisahau bosi wake. Bwana Patel, alikataa katakata aliposikia kaugua maradhi ya akili? Hebu tuone kutatokea nini kwenye kipindi hiki kwa jina **“Mwanzo mpya”.** Tunaanzia palepale tulipomuacha Kapaka na mkewe nyumbani kwao.

**SCENE ONE: KAPAKA NYUMBANI NA FAMILIA YAKE**

1. **SFX:** **BABY MAKING HAPPY GIGGLES**

2. **CHEUPE:** Hata mtoto wetu anafurahia habari njema za wewe kupata tena kazi. Niambie ilitokeaje? Umeajiriwa wapi? Bado utakuwa keshia? Mshahara watakupa pesa ngapi? Ni lini..…

3. **KAPAKA:** Lahaula, taratibu mama, acha nipate funda la maji kwanza, halafu tuketi kisha nikueleze! Hautaamini!

4. **SFX:** **WATER BEING POURED INTO A GLASS**

5. **KAPAKA:** Nilipomaliza kuzozana tu na Patel, karibu nipoteze matumaini, baadae nikaamua kuulizia kazi kwenye duka la jumla linaloangaliana na la Patel. Unajua, wawili hao wamekuwa wakishindania biashara.

6. **CHEUPE:** Naelewa! Hata mimi nilikuwa nikienda kwa Patel kwa sababu ulikuwa ukifanya kazi huko, lakini lile duka jengine lina nafuu.

7. **KAPAKA:** Sawa, acha nimalize basi. Ndiyo nikaenda, kubahatisha, kumbe wananijua! Namueleza

mwenyewe natafuta kazi, na akanimabia: Sawa umepata, nikamuuliza, hivyo tu? Ndiyo nimekuajiri, akasema. Nikachanganyikiwa, na nikajiambia, rahisi hivyo? Haiwezekani. Sasa nikamwambia lakini bado niko kwenye matibabu ya “depression”. Utaniruhusu nifanye kazi?

8. **CHEUPE:** **(excited)** Aha, akasemaje?

9. **KAPAKA:** Hata mimi.

10. **CHEUPE:** **(shocked)** Hapana! Huyo mtu ni mmoja wa matajiri wa nchi hii!

11. **KAPAKA:** Hata mimi nilifikiri hivyo. Kisha akanieleza kisa chake. Kwanza alinieleza kanakwamba amerithi maradhi haya kutoka kwa wazazi wake. Kupitia kuzaliwa na wazazi waliougua. Lakini sasa hali yake ya afya kiakili ni mbaya, kufuatia kutalikiana na mkewe, kwa mujibu wa daktari wake hilo pia linazidi kuchangia. Mbali na usimamizi wa msururu wa maduka makubwa kama yale…

12. **CHEUPE:** Kapaka! Nisingeliamini! Amekutimizia ndoto yako.

13. **KAPAKA:** Pia akanieleza kuwa kwa ajili ya tofauti za kimaumbile, wanaume huathirika zaidi kuliko wanawake na maradhi haya. Na sababu kuu ya wanaume kutaka kujinyonga zaidi kuliko wanawake.

14. **CHEUPE:** Ulimweleza kuwa hata wewe ulitaka kujinyonga?

15. **KAPAKA:** Ndiyo, nilishindwa kumficha. Hata amenieleza jinsi anavyoishi na maradhi haya. Mbali na kunipa kazi mpya, mahojiano yetu yamenitia moyo kurudia hali yangu ya zamani!

16. **CHEUPE:** Namshukuru sana! Sasa, bado utakuwa keshia pia hapo?

17. **KAPAKA:** Ndio, nitakuwa keshia mpya katika “Choice Supermarket”. Bosi wangu mpya anasema kulingana na bidii yangu kazini anatazamia kunipa cheo cha ukeshia mkuu mwakani.

18. **CHEUPE:** **(overjoyed)** Jamani! Sijui niseme nini kuhusu hayo, ni furaha kubwa katika familia yetu. Na siamini kama ni juzi tu tulikuwa tunakupoteza.

19. **KAPAKA:** Cheupe… mkewangu mpendwa. Huu ni mwanzo wetu mpya!

20. **MSIMULIZI:** Bila shaka sio wote wanaopata bahati kama Kapaka. Tafiti zinaonyesha kuwa wengi wanaougua maradhi haya hawakubali kuwa ni wagonjwa, basi huwa ngumu kwao kutafuta matibabu. Tunapoiacha familia hiyo changa ikiogelea kwenye dimbwi la furaha, sasa tunaelekea aliko Chumba ambako amekuwa akikitembelea kikundi hicho kwa majuma ya kuhesabu sasa. Triza,

anayejitolelea kuhudumu hapo ana ujumbe wa mamake Chumba, Malemba.

**SCENE TWO: TRIZA , MALEMBA NA CHUMBA KATIKA "AUTISM CLUB"**

21. **MALEMBA:** Naam, Triza, ulisema una ujumbe wangu. Ni upi?

22. **TRIZA:** Bila shaka ninao, kama ulivyodhania ujumbe unamhusu Chumba.

23. **MALEMBA:** Amezua nini tena mwanangu? Amezidiwa?

24. **TRIZA:** Hapana, mbali na hivyo Chumba amefurahisha kila mtu na kipawa chake cha uchoraji.

25. **MALEMBA:** Unamaanisha nini? Ulijuaje hayo?

26. **TRIZA:** Kama nilivyokueleza awali, wagonjwa wanapokuja hapa, tunajaribu kuwakuza utangamano wao na kuwatia moyo ili waweze kuwa huru. Tunafanya hivyo kupitia muziki, kucheza, maigizo, sanaa, uchoraji, uchongaji, michezo na mambo kama hayo. Nilihitaji siku chache tu kugundua kuwa kijana wako ana kipawa cha uchoraji. Tazama hii ni kazi yake.

27. **SFX:** **PAPERS BEING SHUFFLED SLOWLY… ONE**

**AFTER ANOTHER**

28. **MALEMBA:** **(almost in tears)** Na amechora na kupaka rangi yeye mwenyewe?

29. **TRIZA:** Mwanzoni nilimsaidia, tena kwa kiasi kidogo tu, kwa sababu hakujua matumizi ya kalamu na karatasi. Baadae akaendelea peke yake. Picha si zinavutia, jamani?

30. **MALEMBA:** **(still emotional)** Sio kuvutia pekee, zinapendeza! Chumba, mwanangu leo kweli anachora peke yake. Sasa nimeamini hakuna lisilowezekana.

31. **TRIZA:** Najua bado tuna safari ndefu, lakini ni mwanzo mzuri! Sijawahi kuona haya tangu nije hapa. Afikapo nyumbani basi pia wewe mpe shime, anapopanda hamaki hupoteza makini. Lakini tena, usimshurutishe. Asemapo la, usimlazimishe.

32. **MALEMBA:** Nakupa hakika, Triza. Nimependezwa na kazi yako. Siku hizi amekuwa mtulivu tangu aje huku, na hizi picha zimenipa furaha mno. Nilipoteza nyumba yangu na kila kitu, lakini sasa nina hamu ya kupata nyumba nyengine na mwanangu Chumba. Endelea Triza, nitamchukua baadae.

33. **MSIMULIZI:** Watoto wenye maradhi kama ya Chumba pia wana vipaji, jambo ambalo watafiti na wanasayansi bado

hawajalielewa. Tukiachana na huyo kijana, tunafika majengo ya hospitali ambako Valerie anapatiwa matibabu. Irene amekubaliwa kumtembelea baada ya majuma mawili ya matibabu.

**SCENE THREE: IRENE NA VALERIE KATIKA HOSPITALI**

34. **SFX:** **BIG METAL DOOR BEING OPENED**

35. **IRENE:** **(takes deep breath)** Fyu… hatimaye, wameniruhusu nipite milango yao mikubwa. Sasa muhimu ni kumtafuta Valerie.

36. **SFX:** **MUMBLINGS AND MURMURINGS FROM MENTALLY ILL PERSONS**

37. **IRENE:** Salaale! Sikutarajia kuona wagonjwa wengi hivi. Watu wote hawa wanatoka wapi? Na wanaugua nini? Sawa wadi nambari 11, hapa ndipo alipo Valerie.

38. **SFX:** **DOOR GENTLY KNOCKED**

39. **IRENE:** Valerie, ni mimi, Irene! Niingie?

**SILENCE**

40. **IRENE:** Sawa naja. Wameniambia hakuna tatizo.

41. **SFX:** **SMALL METAL DOOR OPENED WITH**

**SHRIEKING SOUND**

42. **VALERIE/MAHIRO:** Shtuka!!

43. **IRENE:** **(screams in fear)** Wooooooi...

44. **MAHIRO:** **(Laughs uncontrollably)** Hahaha Irene, tumekupata... Tulia wacha wasiwasi.

45. **VALERIE:** Pole rafiki yangu, sikutaka kukushtua lakini daktari alinishawishi. **(laughs a little bit)** Yeye pia ndiye aliyesema usinione. Alisema ninahitaji muda kwa ajili ya matibabu.

46. **MAHIRO:** Kuna tofauti kubwa sana. Valerie bado anasikia sauti hizo lakini anaweza kujizuia. Inaonyesha vile atakavyoweza kukabiliana na hali yake kabisa. Dawa anazotumia zina nguvu kwa hivyo kaa umchunge.

47. **IRENE:** Valerie, tangu ulipoanza haya maradhi sijakuona ukiwa mtulivu jinsi hii.

48. **MAHIRO:** Ni dawa zimemtuliza. Ndiyo sababu ni muhimu kumchunga, kwa sababu anapopata dawa kupita kiasi zitampa madhara mengine. Kama nilivyoahidi, nitahakikisha Valerie amepona kabisa. Hakuna garantii lakini ninatia juhudi zote kwa hilo.

49. **VALERIE:** Nina imani, na nimejitolea kwa lolote litakalonipa afya yangu kamili.

50. **IRENE:** Ni vizuri, Val, vyema kabisa. Lakini daktari, huo umati wote kweli una matumaini ya kupona kama vile Valerie?

51. **MAHIRO:** Kila mgonjwa uliyemuona anatofautiana na mwenzake. Lakini jambo moja ni muhimu kwa wote: iwapo jamii haitawakubali basi afadhali wawekwe humu ndani kuliko kuachwa wakidhulumiwa, kutengwa na kunyimwa haki zao za msingi huko nje.

52. **MSIMULIZI:** Dr. Mahiro anasema kweli. Ameishi miaka mingi akishuhudia dhulma wanazofanyiwa wagonjwa hawa. Lakini mambo hayako mbali kugeuka wakati makamu wa rais ambaye pia ni waziri wa fedha anasoma bajeti ya serikali bungeni.

**SCENE FOUR: M.R ANASOMA BAJETI YA SERIKALI**

53. **SFX: FEET THUMPING AS WHEN LEGISLATORS APPLAUD**

54. **M.R:** Asanteni wajumbe. Sawa, kabla sijamalizia kusoma kitengo kifuatacho naomba mnisikilize kwanza.
**(clears throat)** Kijana wangu hivi sasa anatibiwa

maradhi yanayoitwa “autism”.

55. **SFX:** **UPROAR AND VARIED REACTIONS**

56. **M.R:** La, sihitaji huruma yenu, nihitajicho ni muungano wenu na maelewano. Sote tumekuwa tukipuulizia mbali wagonjwa hawa wa akili lakini wakati wa kuchukua hatua ni sasa. Msinielewe vibaya: hatufanyi haya kwa ajili ya kijana wangu anayeugua. Tunafanya haya kwa sababu ni jukumu letu.

57. **SFX:** **LOUD THUNDEROUS FEET APPLAUSE**

58. **M.R:** Kwa ajili ya hayo, tumeamua kuongeza makadirio ya bajeti yetu kwa ajili ya maradhi haya ya akili, tumeamua tuongeze makadirio ya mwaka jana kwa asilimia 50%. Pesa hizi za ziada zitatumiwa kuongeza madaktari na wauguzi. Tunahitaji kubadilisha mtazamo wetu jinsi tunavyowatibu na kuishi na wagonjwa wa akili.

59. **SFX**: **APPLAUSE**

**<u>HITIMISHO:</u>**

Matangazo hayo ya bajeti yanatutamatishia hadithi hii ya matatizo yanayowafikia wale wenye maradhi ya akili barani Afrika. Hadithi hii imeandikwa na Chrispin Mwakideu. Natumai umeifurahia. Kumbuka

unaweza kusikiliza tena mchezo huu, na hadithi nyengine, kwa kutembelea wavuti wetu dw.de/lbe. Tafadhali tupe maoni yako kuhusu mfumo wa afya nchini mwako. Mpaka tutakapokutana tena. Kwaheri na salamu nyingi kutoka Bonn!